WANAWAKE

# NA KILIMO

NA WARIOBA IGOMBE

# Haki za ardhi mkombozi wa wakulima na wanawake



**WANAWAKE wakiwa shambani wakiendelea na shughuli za kilimo cha bustani ya mboga.**

ARDHI ni uhai walinena wahenga. Neno ardhi, ni mjumuisho wa vitu vyote vilivyopo juu na chini ya uso wa dunia.

Sera na sheria ya nchi hii inatoa fursa kwa makundi yote kuwa na haki ya kumiliki rasilimali mbalimbali ikiwemo ardhi.

Sera na sheria hii imeeleza kuwa makundi yote nchini, ni haki yao kupata na kutumia ikiwa ni pamoja na kunufaika na rasilimali mbalimbali kama vile ardhi hususan kundi la wanawake ambao ndiyo tegemeo kubwa nchini.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ibara 24(1), kila mtu anayo haki ya kumiliki mali, kuwa na haki ya kuhifadhi mali yake kwa mujibu wa sheria zilizopo nchini.

Kutokana na ibara hii ya Katiba, ni wazi kuwa wanawake wana haki sawa ya kumiliki ardhi kisheria kama ilivyyo kwa wanaume na haki hiyo japokuwa jamii nyingi nchini huwaona wanawake kama watu wasiostahili kumiliki ardhi.

Baadhi ya jamii hapa nchini zimekuwa zikimbagua mwanamke katika suala zima la umiliki wa ardhi ikiwa ni pamoja na kutomshirikisha kwenye mambo mbalimbali ya kupitisha maamuzi yanayohusu maombi ya hati miliki hususan za kimila.

Ili kuhakikisha changamoto ya wanawake kunyimwa fursa ya kumiliki ardhi na kutoshirikishwa kwenye maamuzi yanayohusu ardhi Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi (HAKIARDHI) imeamua kumkomboa mwanamke.

Taasisi hii imeamua kumkomboa mwanamke katika jamii kwa kutoa elimu ya kisheria juu ya haki za ardhi maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuelimisha jamii hususani mwanamke mambo muhimu yanayohusu umiliki wa ardhi.

Joseph Chiombola, ni Ofisa Program Mwandamizi wa Hakiardhi anasema kuwa taasisi yake imeamua kuweka utaratibu wa kutoa mafunzo hapa nchini ili kutoa fursa kwa wananchi hususan wanawake kutambua masuala ya haki za ardhi.

Chiombola anasema lengo kuu ni kukuza uelewa kwa jamii juu ya mfumo wa kumiliki ardhi ikiwa ni pamoja na kuitumia kisheria ili wananchi waweze kutetea, kulinda na kudai haki zao kama vile rasilimali ya ardhi kwa ufanisi.

Chiombola ambaye kitaaluma ni Mwanasheria, anasema ardhi ya Tanzania imegawanyika katika makundi matatu.

Anayataja makundi hayo kuwa ni ardhi ya kijiji, hifadhi na jumla ambapo anafafanua kuwa ardhi ya kijiji ni ile iliyo ndani ya mipaka ya kijiji.

Ardhi ya hifadhi ni ile iliyotengwa kwa ajili ya matumizi maalum kama vile hifadhi za taifa za wanayapori,milima,misitu na barabara. Ardhi ya jumla ni ile iliyobaki baada ya kuondoka kijiji na hifadhi kwa mujibu wa sheria za nchi.

Anaeleza kuwa kwa mujibu wa sheria za Katiba ya nchi kifungu cha 3(2) za Sheria za Ardhi namba tatu na tano kinaainisha kuwa mwanamke ana haki ya kupata, kumiliki, kutumia, kuigawa au kuiuza kama vile mwanaume alivyo na haki hiyo.

Chiombola anaeleza kuwa kutokana na changamoto kutoka kwa baadhi ya wananchi hususani wanawake kutojua sheria za haki ya ardhi taasisi yake imeamua kutoa elimu juu ya haki hiyo ili jamii iweze kuelimika na kuepuka migogoro.

"Baada ya kufanya utafiti wa kina imebainika kuwa baadhi ya watu hususan wanawake hudhulumiwa ardhi yao kwa kutojua haki za ardhi, kitendo ambacho kimekuwa kikichochea migogoro ya ardhi nchini," anasema Chiombola.

Mtaalamu huyo wa sheria anaeleza kuwa, haki ya mwanamke kwenye suala zima la kumiliki ardhi ni pamoja na kumiliki ardhi na kumlinda dhidi ya mtu yeyote anayeweza kuchukua uamuzi wa kuichukua ardhi yake kwa kutumia mabavu.

Cuthbert Tomitho, Mkurugenzi Mtendaji wa HAKIARDHI anasema taasisi yake ilianzishwa mwaka 1994 kwa lengo la kutafiti, kuibua na kuendeleza mijadala mbalimbali inayohusu haki za ardhi za wazalishaji wadogo hapa nchini.

Tomitho anasema lengo la taasisi yake ni kuhakikisha haki za jamii ya wakulima na wafugaji ambao ni wazalishaji wadogo hususan wanaoishi maeneo ya vijijini, zinatambuliwa, zinazingatiwa na kulindwa kwa mujibu wa sheria.

"Tangu kuanzishwa kwa taasisi hii, tuko katika mstari wa mbele kuibua na kuendeleza mijadala juu ya sera, sheria na mikakati yenye tija kwa taifa katika suala zima na kutetea haki za wazalishaji wadogo hususan wakulima na wafugaji," anasema Tomitho.

Anaeleza kuwa mbali na wazalishaji wadogo ambao ni wakulima na wafugaji kupewa elimu ya kutambua sheria na haki za ardhi, lakini pia taasisi imekuwa ikiwasaidia Watanzania wanyonge kujua sheria za haki za ardhi.

"Tangu kuanzishwa kwa taasisi hii tumewasaidia sana wanyonge kupata haki zao kwa kuibua mijadala mbalimbali inayohusu haki ardhi, hali iliyofanya mamlaka husika kuchukua na kutoa uamuzi unaostahili," anasema Tomitho.

Tomitho anaeleza dhamira kuu ya taasisi hiyo ni kujenga jamii yenye watu wenye mwamko wa kutambua, kufuatilia, kutetea na kudai haki zao za ardhi ikiwa ni pamoja na rasilimali nyinginezo pale zinapokwapuliwa kwa manufaa ya taifa.

"Lengo la hakiardhi ni kukuza ufahamu kwa jamii juu ya masuala ya ardhi, kuimalisha mifumo ya utoaji wa maamuzi juu ardhi na kuwezesha ushiriki wa wananchi wanyonge kudai na kulinda haki zao za ardhi,"anasema Tomitho.

Anataja maeneo yanayoongoza kwa migogoro ya ardhi iliyosababishwa na dhuluma kutokana na watu kutojua sheria za ardhi hususan wanawake ni pamoja na Kilolo mkoani Iringa na baadhi ya maeneo ya wilaya mkoani Morogoro.

Ili kuhakikisha dhamira ya taasisi hii inafanikiwa wamekuwa wakiandaa warsha pamoja na kushiriki makongamano mbalimbali ya wanawake na kutoa elimu ya haki ardhi ili kumkomboa mwanamke dhidi ya unyanyasaji na dhuruma.

Katika kongamano lililofanyika hivi karibuni Kilombero mkoa wa Morogoro kundi la wakulima wadogo ikiwa ni pamoja na wanawake ambao ndiyo wazalishaji wakubwa wa uchumi hapa nchini walipata fursa ya kupata elimu ya haki ardhi.

Katika kongamano hilo ambalo lilihudhuliwa na wanawake kutoka maeneo mbalimbali ya wilaya ya Kilombero taasisi hii ilitoa elimu kwa wananchi juu ya haki za ardhi, mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja sheria za ardhi.

Wakulima wadogo hususani wanawake walitumia fursa hiyo kupata elimu juu ya mabadiliko ya tabianchi, sheria za ardhi na kuwajengea uwezo wa kuwa jasiri kupigania haki yao katika jamii zao.

Mariamu John ni miongoni mwa wanawake walioshiriki kongamano hilo anasema kitendo cha baadhi ya watendaji wa serikali kuwa wabinafisi kwa kutanguliza masilahi yao kumechangia migogoro mingi ya ardhi katika jamii nchini.

Kutokana na kauli hiyo, Kamishina wa Ardhi nchini, Mary Makondo, amewataka wanawake kuwa na ujasiri wa kudai haki zao pamoja na kumiliki ardhi kwani kufanya hivyo kutawakwamua na umaskini wanaokabiliana nao kila siku.

Anasema ardhi ni mtaji na mhimili mkubwa unaokuza uchumi wa wanawake nchini hivyo ni wajibu wa kila mwanamke kutambua umuhimu huo kwani kufanya hivyo taifa litakuwa na maendeleo yatakayochangiwa na kazi za wanawake.

"Napenda kutumia fursa hii kuwata wanawake wote hapa nchini kuwa na ujasiri utakaowasaidia kumiliki ardhi iliyopimwa kisheria wao wenyewe kwani kufanya hivyo kutawajengea uwezo wa kujiunua kiuchumi "anasema Makondo.

Makondo anasema serikali imefanya maboresho katika sera ya ardhi kwa lengo la kuhakikisha wanawake wanalindwa ambopo aliwataka wadau wa ardhi nchini kushirikiana na serikali kutoa elimu ili kuielimisha jamii juu ya mila potofu.

Anasema serikali imeweka mpango utakaohakikisha ardhi yote inapimwa kwa mujibu wa sheria na kueleza kuwa serikali kwa kushirikiana na wadau wa ardhi nchini, wamesaidia wanawake Wilaya ya Kilombero kumiliki ardhi.

Mbali na Kilombero, pia kuna Wilaya za Ulanga na Malinyi za Mkoa wa Morogoro ambapo baada elimu kutolewa, wanawake waliamua kuwa na ujasri na kuamua kumiliki ardhi kwa asilimia 40 tofauti na asilimia mbili za miaka ya nyuma.

Kwa upande wake, Mratibu wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo kuondoa umasikini na matatizo ya binadamu nchini (OXFAM), Naomi Shadrack, anasema matumizi ya ardhi kwa mwanamke ni aslimia 52 barani Afrika.

Shadrack anasema kitendo cha mwanamke kumiliki ardhi, kunaongeza thamani na hadhi yake ya kujiinua kiuchumi utokanao na sekta ya kilimo na kumuwezesha mwanamke kuwa na ulinzi dhidi ya ukatili wa kijinsia.